

HOTUBA YA MHESHIMIWA MAMA SALMA KIKWETE
KATIKA CHAKULA CHA JIONI CHA KUCHANGIA MIRADI
YA ELIMU NA AFYA NCHINI. TAREHE 26 NOVEMBA
2010, VALENCIA, SPAIN.

Mabibi na Mabwana,

Napenda kuanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema kwa kutuwezesha kushiriki katika hafla hii tukiwa wenye afya njema. Pia nitumie fursa hii kuwashukuru wote mliohudhuria hafla hii. Kwani kuwepo kwenu kunadhihirisha jinsi mnavyothamini ndugu zenu wa Tanzania kwa kuchangia juhudi zao katika afya na elimu.

Aidha kwa nafasi ya pekee kabisa, nimshukuru Bibi **Isabel Quintanilla**, timu yake na wote waliofanya kazi usiku na mchana ili kufanikisha hafla hii ambayo ni kilele cha juhudi

kubwa mlizofanya ili kuleta mabadiliko chanya kwa ndugu zetu wenye mahitaji mbalimbali.

Kwa niaba ya Watanzania wenzangu, hususan wale wanaolengwa na huduma mnazo zichangia, napenda kutoa shukrani za dhati kabisa kwa jamii ya Valencia na watu wote waliotoa michango yao.

Baada ya kutoa shukrani hizo, ningependa nianze hotuba yangu kwa kuwaeleza machache juu ya elimu ya mtoto wa kike nchini Tanzania. Nchini kwetu elimu imepewa kipaumbele cha kipekee miongoni mwa malengo ya maendeleo ya milenia. Mpango wa maendeleo ya elimu umewekewa malengo mahususi katika Dira ya Maendeleo ya mwaka 2025 (Development Vision 2025). Dira yetu imeweka suala la elimu kuwa ni moja ya nguzo muhimu ambayo inahitajika katika kuleta maendeleo ya watanzania.

Moja ya malengo ya Mpango wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini nchini (MKUKUTA), ni kutoa fursa sawa katika elimu ya msingi na sekondari kwa watoto wa kike na wakiume. Hata hivyo, watoto wa kike wamekuwa wakikosa fursa hizo kutokana na sababu mbali mbali, zikiwemo za kihistoria hususan siku za nyuma katika jamii nyingi, mtoto wa kike alinyimwa nafasi ya kwenda shuleni na kuonekana kama ni mtu wa kusaidia kazi za nyumbani na kulea familia. Katika siku za karibuni hadi sasa watoto wakike wamekuwa wakishindwa kuendelea na masomo kutokana na matatizo mbalimbali ikiwemo ndoa za umri mdogo, mimba za utotoni, na umaskini unaowafanya washindwe kupata mahitaji muhimu ya shule.

Aidha, sekta ya elimu kwa ujumla inakabiliwa na matatizo mbalimbali yakiwemo upungufu wa vifaa vya kufundishia na majengo ya maabara, upungufu wa walimu, na mabweni kwa watoto wa kike kwa shule za sekondari. Mambo yote

haya yanahitaji juhudi za pamoja ili kuzikabili. Mfano huu ulioonyeshwa na watu wa Valencia ni wa kuigwa, kwani naamini kuwa ikiwa kila mmoja wetu atatekeleza jukumu lake hakuna mtoto atakeshindwa kwenda shule kwa kukosa ada au mahitaji binafsi. Watoto wote ni watoto wa dunia yetu na nimefarijika na jinsi mlivyoguswa na mahitaji yao na kuamua kufanya jambo hili. Nawashukuruni sana.

Mabibi na Mabwana

Mimi nikiwa kama mke wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mwalimu na mzazi, ninaguswa sana na changamoto zinazowakabili watoto wa kike katika kupata elimu bora. Kwa sababu hiyo nilianzisha taasisi ya Wanawake na Maendeleo (WAMA). Kupitia taasisi hii tumekuwa tukitoa fursa kadhaa za elimu ya sekondari; Tumejenga mabweni ili kuweka mazingira salama ya utoaji wa elimu; tumetoa vifaa mbalimbali vya uboreshaji wa elimu vikiwemo umeme wa kutumia mionzi ya jua (solar power),

vitabu na michezo; Tumejenga shule maalum kwa ajili ya watoto wakike ambao ni yatima na wenye mahitaji; Halikadhalika tumejenga shule katika kata ambayo haikuwa na shule ya sekondari, ili kuongeza fursa za elimu.

Mabibi na Mabwana

Napenda kuchukua fursa hii kuwaomba na kukualikeni nyote muendeleo kuunga juhudi za WAMA, Juhudi za Mhe. Mwantumu Mahiza kwani bado watoto hawa wanakabiliwa na matatizo na wale wachache ambao wanapata msaada bado wanahitaji kupata msaada zaidi ili waweze kuendelea mbele.

Mabibi na Mabwana

Baada ya kusema hayo, niwashukuru tena na kuwatakia furaha katika chakula hiki cha jioni.

Ahsanteni kwa kunisikiliza